BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Tano – Tarehe 21 Mei, 2024**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka 2024/2025.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa Mwaka 2024/2025.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

258. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Kumekuwa na tabia ya Jeshi la Polisi, Kitengo cha Usalama Barabarani kuwaweka ndani madereva wa vyombo vya moto hasa vya maringi mawili bila ya kuwasomea makosa yao na kisha kuwapiga faini bila ya kuwasomea makosa yao madereva hao.

(a) Je, kwa kiasi gani vitendo hivi vinakiuka misingi ya haki dhidi ya madereva hao.

(b) Ni ipi kauli ya Serikali ya kuwajengea imani wananchi hao kwa Serikali yao.

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

57. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Pamoja na kazi nzuri ya Serikali ya Awamu ya Nane katika kuweka mazingira ya miji yetu kuwa safi, hivi karibuni kumejitokeza ongezeko la utupaji wa taka za plastiki usiokuwa sahihi katika maeneo mbali mbali ya Mji wa Zanzibar. Kwa kuwa sheria zetu za usimamizi wa mazingira zipo.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza kasi ya utekelezaji wa sheria za usimamizi wa mazingira ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na taka za plasitiki.

(b) Kwa kuwa wafanyabiashara wengi wanayo mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku katika maduka yao, ni lini Serikali itaanzisha operesheni maalumu ya duka kwa duka ili kuwabaini na kuwachukulia hatua wafanyabiashara wanaovunja sheria na kukaidi maagizo ya Serikali.

**<u>Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:</u>**

165. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Miongoni mwa changamoto kubwa ya utumishi wa umma hapa Zanzibar ni pamoja na watumishi hawa kutoutumia ipasavyo muda wanapokuwepo kazini kwa hujishughulisha na mambo yasiyohusiana na masuala ya kazi, bila ya kujali kuwa wanafanya makosa na uzembe kazini.

Je, kwa kiasi gani uzembe wa kutotumia muda ipasavyo kwa watendaji wa Serikali (Time Management), unakwaza na kuzorotesha maendeleo ya jamii yetu.

**<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>**

41. MHESHIMIWA MARYAM THANI JUMA (Jimbo la Gando) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa kuwa suala la kulipa kodi linahitaji uhiari, mwamko wa wananchi na uzalendo wa mtu.

Je, ni kwa namna gani taasisi za kodi hasa Mamlaka ya Mapato ya Zanzibar (ZRA) zinawafikia wanafunzi wa maskulini ili kuanzisha vilabu (club) vya kodi kwa lengo la kuwahamasisha vijana juu ya umuhimu wa kulipa kodi.

**<u>Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:</u>**

156. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Serikali imeamua kulitangaza eneo la Kiuyu Maziwa Ng’ombe kuwa ni eneo la uwekezaji na tayari baadhi ya miundombinu kama vile barabara imeshawekwa.

(a) Je, ni hatua ipi iliyofikiwa hadi sasa ya kulikamilisha eneo hili kuwa la uwekezaji.

(b) Je, ni wawekezaji wangapi tayari wameshadhamiria kuja

kuwekeza katika eneo hili.

(c) Je, ni ipi kauli ya Serikali kuhusiana na eneo hili.

## Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

160. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Aamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Tathmini iko vipi juu ya muendelezo wa jengo la kihistoria la Nguli wa muziki Afrika Mashariki na Kati na dunia kwa ujumla, Siti binti Saad.

## Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

28. MHESHIMIWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Utekelezaji wa Sera mpya ya Elimu Zanzibar ulianza rasmi mwaka 2023 kwa skuli za maandalizi na msingi.

(a) Je, ni sababu gani zilizochangia kuchelewa kupatiwa mafunzo walimu wanaosomesha madarasa hayo.

(b) Ni sababu gani zilizochangia hadi leo kuchelewa na kukosekana kwa vifaa muhimu vya kutendea kazi kama vile mihutasari, vitabu vya kiada na ziada kwa madarasa hayo.

(c) Je, hatuoni kuwa kukosekana kwa vifaa hivi muhimu vya kufundishia na kujifunzia ni kurudisha nyuma kasi ya utekelezaji wa mtaala huu mpya.

173. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Ni upi mpango wa Wizara yako wa kuwapatia wanafunzi wetu Maktaba Mtandao ili kuondokana na tatizo la uhaba wa vitabu vya kusomea na kujifunzia.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

140. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Katika siku za hivi karibuni kumejitokeza wananchi kula samaki anaejulikana kwa jina la kasa, hali iliyopelekea vifo kwa watu wengi kufariki kwa pamoja ambapo maeneo yaliyoathirika na kutokea kwa vifo hivyo ni pamoja na Matemwe, Micheweni na Kisiwa Panza.

(a) Je, suala hili linaeleweka vipi katika Serikali yetu.

(b) Je, Serikali itachukua hatua gani ili kudhibiti hali hiyo.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

171. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Aamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

(a) Kwa kiasi gani kilimo cha kisasa (smart agriculture) kinaweza kuwa na mchango mkubwa wa kuwakomboa wakulima wetu, hususan wakulima wadogo wadogo.

(b) Kwa vipi Serikali imejiandaa katika kuwapa msukumo wakulima, ikiwa ni pamoja na wakulima wadogo wadogo wanaodhamiria kujikita katika kilimo cha kisasa.

245. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Mahitaji makubwa ya nishati ikiwemo kuni na mkaa yamekuwa yakisababisha uharibifu mkubwa wa misitu.

Je, Serikali ina mbadala gani unaotekelezeka wa kupambana na uharibifu huu mkubwa wa misitu.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

31. MHESHIMIWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Tunaipongeza Serikali kwa hatua nzuri ya kuiletea nchi yetu maendeleo kupitia sekta mbali mbali ikiwemo ya maji na nishati. Katika maendeleo hayo ni pamoja na mradi mpya wa maji nchini uliolenga kuwatua wanamama ndoo za maji kichwani. Hata hivyo, kuna idadi kubwa ya wananchi waliopitiwa na mradi huu katika maeneo tofauti nchini ikiwemo Masingini lakini hadi leo wananchi hao bado hawajaunganishiwa huduma hii muhimu majumbani, ingawa tayari wameshatekeleza hatua zote zinazostahiki.

(a) Je, kuna sababu zipi za msingi ambazo zinazopelekea hali hii.

(b) Ni utaratibu gani uliowekwa ambao utahakikisha wananchi wote waliopitiwa na mradi huu wananufaika na huduma hii.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka 2024/2025.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka 2024/2025.

Zanzibar,
21 Mei, 2024.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA